



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOSA



Unapojibu Tafadhari Taja,

Kumb. Na KDC/L.20/22/54

Tarehe 12/2/2024

Mkurugenzi Mtendaji (W),
S. L. P 65,
KILOSA.

YAH: TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI YA DEREVA WA MKATABA

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa anakaribisha maombi ya kazi ya udereva wa mkataba kutoka kwa Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi nne (4) kama ilivyoainishwa kwenye tangazo hili.

1.0 DEREVA NAFASI 4

1.1 SIFA ZA MUOMBAJI

- Awe na cheti cha kidato cha nne (IV)
- Awe na leseni ya daraja la C au E ya uendeshaji wa magari ambayo imefanyiwa kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali
- Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na chuo cha mafunzo ya Ufundi stadi (VETA), NIT au chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.

1.2 MAJUKUMU YA KAZI

- Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari
- Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari
- Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali
- Kujaza na kutunza taarifa zote katika daftari la safari
- Kufanya usafi wa gari

1.3 MSHAHARA

Mwombaji atakaefanikiwa kuajiriwa mshahara kwa mwezi utakuwa ni makubaliano kati yake na Mwajiri.

1.4 MASHARTI YA JUMLA

- i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri kuanzia miaka 18 – 45
- ii. Waombaji wote waambatishe nakala ya cheti cha kuzaliwa
- iii. Barua ya muombaji ioneshe anuani anayotumia kwa sasa pamoja na namba za simu ikiambatana na:-
 - a) Nakala za vyeti vya taaluma
 - b) Nakala za vyeti vilivyothibitishwa na Mwanasheria/Wakili ambavyo ni vyeti vya kidato cha nne na kidato cha sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika
 - c) Maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed CV) yenye anauani na namba za simu zinazopatikana pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika
 - d) Picha mbili (2) za "Passport Size" za hivi karibuni
 - e) Kitambulisho au namba ta Kitambulisho cha Taifa (NIDA)
- iv. Waombaji wote waliowahi kupatikana na kosa la jinai hatafikiriwa
- v. **"Testmonial", "Provisional Results", Statement of Result"** hati za matokeo ya kidato cha nne (**FORM IV RESULTS SLIPS**) **HAVITAKUBALIWA**
- vi. Uwasilishaji wa taarifa za sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria waombaji wenye sifa wanatakiwa kutuma maombi kupitia Posta kwa anuani ifuatayo:-

**Mkurugenzi Mtendaji (W),
Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa,
S.L.P 65,
KILOSA.**

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 26 Februari, 2024 saa 9:30 Alasiri.

NB: Tangazo hili pia linapatikana katika tovuti ya Halmashauri www.kilosadc.go.tz

Michael J. Gwimile
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
KILOSA

